

**TAARIFA FUPI YA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI KATA YA LUHUWIKO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 06-05-2017**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017**, Ninayo furaha kubwa sana kukukaribisha wewe pamoja na msafara wote uliofuatana nao hapa katika Kata ya Luhuwiko, nasema karibu sana na ujisikie upo nyumbani.

**Ndugu, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017**, Mradi huu wa Shule ya sekondari Luhuwiko ulianza kujengwa Januari 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2017

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017**,lengo la mradi huu ni kupunguza msongamano wa wanafunzi waliopo katika shule za sekondari za Mbambi, Makita na Mbinga pia kupunguza umbali kwa wanafunzi wanao toka maeneo ya mbali kama vile Masasi,Lusaka,Lusonga,Tugutu na Bethrehemu.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017**, hadi kukamilika kwa mradi huu utagharimu kiasi cha tshs **61,506,000/=**, kati ya fedha hizi Tshs **23,000,000/=** ni michango ya Wadau na nguvu za Wananchi na Tshs **38,506,000**. fedha kutoka Serikali kuu (Ruzuku ya Maendeleo), pia vifaa vyote vya Viwandani kwaajili ya ukamilishaji wa ujenzi vimeshanunuliwa.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017**, Wananchi wa Kata ya Luhuwiko waanaamini kwamba Mafanikio ya Viwanda yanategemea Jamii iliyoelimika ,hivyo Wananchi wanaunga mkono kauli mbiu inayosema. *“Shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu”*

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017**, Baada ya taarifa hii, kwa heshima na taadhima, sasa nakuomba uweke jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Sekondari iliyopo Kata ya Luhuwiko.

Ni mimi,

**ANSILA M. KUMBURU  
AFISA MTENDAJI  
KATA YA LUHUWIKO**

**KWA NIABA YA WANANCHI WA KATA YA LUHUWIKO**